MRADI WA FOLUR TANZANIA

# Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Visumbufu

**Utangulizi**

FOLUR ni Mradi unaojihusisha na masuala ya Mifumo ya Chakula, Matumizi Endelevu ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili, Mandhari na Misitu. Mradi unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) na kutekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Idara ya Misitu na Nyuki kwa ushirikiano na WWF. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2024/25–2028/29).

Mradi unatekelezwa katika Kongani mbili za Kilombero (Tanzania Bara) na Kaskazini Unguja A na B (Zanzibar) kwa kusimamiwa na Ofisi kuu ya Mradi iliyopo Dodoma, Jengo la Wizara ya Maliasili na Utalii, mji wa Serikali Mtumba. Pia mradi una ofisi za Konga; Kongani ya Kilombero ofisi zipo Halmashauri ya Mlimba na Kongani ya Zanzibar ofisi zipo jingo la Idara ya Misitu, mtaa wa Maruhubi.

Lengo kuu la mradi ni kukuza mbinu jumuishi zinazochanganya uzalishaji endelevu wa chakula kwa kuimarisha minyororo ya thamani isiyochochea uharibifu wa misitu hususan zao la mpunga, pamoja na mipango ya utunzani na urejeshaji wa mandhari, ili kulinda na kuendeleza mifumo ya ikolojia. Katika kipindi cha utekelezaji, mradi wa FOLUR unatarajiwa kuchangia katika kuboresha uzalishaji wa mpunga, kulinda rasilimali za asili, na kuimarisha ustawi wa jamii kwa njia endelevu na jumuishi.

**Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Visumbufu**

Mpango huu wa Usimamizi Shirikishi wa Visumbufu (Pest Management ESMP) unalenga kuhakikisha Afya na Usalama wa Jamii na mazingira kwa kuhakikisha kuna udhibiti wa kiwango cha juu wa athari hasi zinazoweza kujitokeza kutokana na udhibiti wa Visumbufu hasa kwa matumizi ya Viuatilifu na Mbolea. Mradi unafuata vigezo vya Kimataifa vya Usalama wa Jamii na Mazingira vya Taasisi ya WWF. Vigezo hivi vinalenga kubaini athari kabla hazijajitokeza, kuziepuka athari hizo au kupunguza madhara ya athari hasi zinazoweza kuathiri wanajamii au mazingira husika.

Mradi hautaruhusu kununua au kutumia viuatilifu vinavyotambuliwa na Shirika la Afya Duniani kuwa ni Hatari kwa Matumizi. Badala yake, mradi utahakikisha viuatilifu vinavyotumika ni salama kwa kuidhinishwa na Taasisi mahususi, na vinatumika kwa kufuata kanuni za usalama ikiwa ni pamoja na vifaa vya kujikinga kama glovu, barakoa, na mavazi maalum. Hii ni ili kulinda afya ya mkulima, jamii, na mazingira.

Mradi pia utafuata miongozo ya kimataifa ya matumizi sahihi ya viuatilifu, ili kuhakikisha matumizi yake hayaleti madhara kwa watu, mifugo, mazao, na mazingira.

Aidha, wakulima watafundishwa jinsi ya kutumia viuatilifu kwa usahihi, na pia watapatiwa elimu ya kutumia njia mbadala zisizo za kemikali kudhibiti wadudu, kama vile kilimo bora na mbinu za kudhibiti wadudu kwa pamoja (IPM)**.** Ni muhimu kuelewa kuwa hata kama viuatilifu na mbolea zimeidhinishwa, si kila mtu anajua kuzitumia vizuri. Ndiyo maana mradi utatoa mafunzo kwa wakulima na wadau wengine ili kuhakikisha matumizi salama na yenye tija.

**Athari zinazoweza Kujitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Mradi**

## I. Athari Chanya (Zenye Faida kwa Jamii na Mazingira).

i. Kuimarishwa kwa upangaji na usimamizi jumuishi wa matumizi ya ardhi na maji katika maeneo lengwa.
ii. Urejeshaji Uoto na Mandhari wa ardhi zilizoharibika katika maeneo ya kipaumbele.
iii. Usimamizi jumuishi na endelevu wa maeneo yenye thamani kubwa ya uhifadhi (HCV).
iv. Kurejesha ubora wa maji kwa matumizi ya binadamu na matumizi mengine.
v. Kuboreshwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji (VLUPs) na kupunguza migongano ya matumizi.
vi. Kuongeza uelewa na umuhimu wa uhusiano wa uhifadhi wa mazingira na uboreshaji wa kilimo cha mpunga.
vii. Kupungua kwa matukio ya mashambulizi kutoka kwa wanyamapori kama viboko na mamba dhidi ya binadamu na mali zao.

## II. Athari Hasi na Mapendekezo ya Utatuzi

| Athari | Utatuzi |
|---|---|
| **Athari kwa Afya ya Binadamu**<br>Changamoto za **moja kwa moja**; Wafanyakazi wa mashambani wako katika hatari kubwa ya kuathiriwa, ikiwa ni pamoja na athari za sumu, muwasho wa ngozi na macho, pamoja na matatizo ya kupumua.<br><br>Changamoto za Matumizi ya **muda mrefu** ya viuatilifu yanaweza kusababisha magonjwa kama saratani, matatizo ya homoni, matatizo ya mfumo wa neva, na matatizo ya uzazi. | • Kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi salama ya viuatilifu<br>• Kuhakikisha matumizi ya vifaa kinga binafsi (PPE) kama glovu, barakoa, na mavazi maalum<br>• Kukuza matumizi ya mbinu mbadala kama **IPM (Udhibiti Shirikishi wa Wadudu)**<br>• Kuhamasisha usafi wa chakula na maji (kuosha mazao, kutumia maji salama)<br>• Kutoa elimu ya dalili za sumu na hatua za haraka za matibabu |
| | |

| | |
|---|---|
| **Athari za Kiuchumi kwa Wakulima**<br><br>Gharama kubwa ya kununua viuatilifu huongeza mzigo wa kifedha. Aidha, kuzoea kwa wadudu au mazao (resistance) kunaweza kulazimisha matumizi ya kemikali zaidi au ghali zaidi. Athari za kiafya pia husababisha kupotea kwa muda wa kazi na gharama kubwa za matibabu. | • Kukuza matumizi ya mbinu nafuu na endelevu kama IPM<br>• Kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ili kupunguza matumizi kupita kiasi<br>• Kuimarisha vikundi vya wakulima kwa ununuzi wa pamoja ili kupunguza gharama<br>• Kutoa elimu ya usimamizi wa fedha na uzalishaji<br>• Kuhamasisha matumizi ya mbinu zisizo za kemikali. |
| **Masuala ya Usalama wa Chakula**<br><br>**Athari:**<br>Mabaki ya viuatilifu kwenye mazao yanaweza kuathiri biashara. Viwango vikubwa vinaweza kusababisha mazao kukataliwa sokoni. | • Kufundisha wakulima kuzingatia muda wa kusubiri kabla ya kuvuna (pre-harvest interval)<br>• Kuhamasisha matumizi sahihi ya viuatilifu vilivyoidhinishwa<br>• Kufuatilia viwango vya mabaki ya viuatilifu kwenye mazao<br>• Kutoa elimu juu ya viwango vya soko na ubora wa mazao<br>• Kukuza kilimo hai au matumizi madogo ya kemikali |
| **Ukosefu wa Usawa wa Kijamii**<br><br>**Athari:**<br>Kutokea kwa ukosefu wa usawa pale wakulima wadogo wanapokosa mafunzo na kufanya kazi katika mazingira duni bila vifaa vya kujikinga. | • Kuhakikisha mafunzo yanawafikia wakulima wote bila ubaguzi (wanawake, vijana, wadogo)<br>• Kutoa au kuwezesha upatikanaji wa vifaa kinga kwa bei nafuu<br>• Kukuza ushiriki jumuishi katika mafunzo na maamuzi ya mradi<br>• Kuimarisha vikundi vya wakulima kwa msaada wa pamoja<br>• Kufuatilia usawa wa upatikanaji wa rasilimali na huduma |

| | |
|---|---|
| **Uchafuzi wa Mazingira**<br><br>**Athari:**<br>Matumizi ya viuatilifu na mbolea yanaweza kusababisha uchafuzi wa maji na udongo vifo vya samaki na viumbe wengine wa majini. Uchafuzi wa udongo unaweza kuharibu viumbe hai wadogo wa udongoni. | • Kukuza matumizi sahihi na ya kiwango cha viuatilifu na mbolea<br>• Kuweka maeneo kinga karibu na vyanzo vya maji (buffer zones)<br>• Kufundisha uhifadhi salama na utupaji wa vifungashio vya kemikali<br>• Kufuatilia ubora wa maji na udongo mara kwa mara<br>• Kukuza kilimo hifadhi na matumizi ya mbolea asilia |

**Uwasilishaji wa Malalamiko**

Iwapo kutakuwa na malalamiko kutoka kwa mtu binafsi, kundi au jamii kutokana na baadhi ya shuguli zinazotekelezwa na mradi, muhusika atatakiwa kuwasilisha malalamiko hayo kwa moja ya njia zilizoainishwa hapa chini. Malalamiko husika yatafanyiwa kazi na muhusika atapewa mrejesho kulingana na aina ya lalamiko.

| **Ngazi ya Uwasilishwaji** | **Namna ya Kuwasilisha** |
|---|---|
| Jamii | Baada ya Kutolewa elimu ya miongozo ya mradi, kijiji kitapendekeza jina la mtu, au taasisi iliyopo kijijini mfano CBO/Kanisa/Msikiti ambao utaweza kuwa sehemu ya awali ya kuanzisha mchakato wa Malalamiko. Kitakachokusanywa kitawakilishwa kwenye mradi au wizarani ili kuweza kufanyiwa kazi.<br><br>Mwasiliano ya Muhusika<br>Jina (Mtu au Taasisi)…………………………………….<br>Namba ya simu ……………………………………..<br><br>*Mradi utahakikisha kila kilichowasilishwa kimeingizwa kwenye fumu mahususi ili kipate kufanyiwa kazi na mrejeshwo kutolewa.* |
| Kongani/Halmashauri | Ofisi za Kongani zinaweza pia kutumika kama fursa ya kuanzisha mchakato wa kuwakilisha malalaminko. Kitakachopatikana hapa kitawasilishwa kwa Afisa Muhusika Ngazi ya Makao Makuu au Wizarani.<br><br>Mawasiliano.<br><br>Mlimba<br>Joseph Mgana, +255787958877 josephmgana@gmail.com |

| | |
|---|---|
| | Zanzibar<br>Miza Khamis +255777332223 mizakhamis@gmail.com<br><br>*Mratibu akiisha kupokea nia ya kuwasilisha lalamiko, atawasiliana na afisa anaeyeshughulikia malalamiko ngazi ya Makao Makuu au Wizara ili mchakato wa Kuanzisha lalamiko rasmi uanze.* |
| ***Ikumbukwe, Ili lalamiko lifanyiwe kazi lazima kujazwe fomu mahususi inayotolewa na Afisa Husika Ngazi ya Makao Makuu au Wizarani kulingana na aina ya lalamiko. Ngazi ya Kongani na Kijiji ni kwaajili ya kumsaidia Muhusika kupata mawasiliano ya Afisa Husika Ngazi ya Makao Makuu au Wizara.*** | |
| Ngazi ya Kitaifa | Malalamiko yawasilishwe kwenye Ofisi za Makao Makuu ya Mradi kupitia Mratibu wa Masuala ya Jinsia na Mazingira/Afisa anaeshughulika na Malalamiko.<br><br>Revocatus Kadoshi<br>(+255765 456 218 revocatusg@gmail.com)<br>au<br>Mratibu wa Mradi<br>(wanjala.mgaywa@maliasili.go.tz/+255755690187)<br>Au<br>MkurugenziIdara ya Misitu na Nyuki – Wizara ya Maliasili na Utalii (dfob@maliasili.go.tz/+255755578057) |
| Kimataifa | Email: SafeguardsComplaint@wwfus.org<br><br>https://secure.ethicspoint.com/domain/media/en/gui/59041/index.html. |